# Learning by Ear 2009
# Children's Rights Series
# 04 Street children

**Topic:** **Street children and the dangers they face**

**Author:** **Sam Olukoya (Nigeria)**

**Editors:** **Sandrine Blanchard / Yann Durand**

**Translator:** **Anne Thomas**

**Kisuaheli** **Eric Ponda**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| IN/OUTRO | X | | Unimportant | |
| Narrator | | X | Ca. 25 | |
| Princess Joel | X | | 13 | English |
| | | | | |

| LbE Soundtrack |
|---|

**INTRO:**

Hujambo mpenzi msikilizaji popote ulipo na karibu kwa makala ya nne kuhusu haki za watoto na juhudi za kudumisha amani. Leo tunakutana na Princess Joel ambaye ni Chokora pipa au Mtoto wa kurandaranda mitaani.

Hakuna ripoti rasmi iliyotolewa kuhusu idadi kamili ya watoto wanaoranda randa mitaani kote duniani lakini inakisiwa kuwa kati ya watoto milioni 40 na

60 wanaishi mitaani huku nusu ya idadi hiyo wakiwa wanapatikana barani Afrika.

Princess aliishi kama mtoto omba omba katika barabara za mji mkuu wa Lagos, nchini Nigeria kwa zaidi ya mwaka mmoja. Barabara za mji huo zinafahamika kuwa hatari kwa watu wazima na hata watoto. Watu hushikwa kabari na kuporwa mali zao au hata kuuawa hadharani. Princess ameshuhudia visa hivi tangu akiwa na umri wa miaka 13. Aliweza kuokolewa na shirika moja lisilo la kiserikali na leo anatuelezea maisha yake kama mtoto omba omba na jinsi alivyopoteza maisha yake ya utotoni.

| **Report** |
|---|

**Narrator:**

Princess Joel alizaliwa katika kijiji kimoja yapata umbali wa kilomita 600 Kusini Mashariki mwa mji mkuu wa Lagos. Akiwa na umri wa miaka 13 aliamua kutoroka umaskini uliokithiri katika sehemu za mashambani alikoishi na kuhamia mjini. Bado anakumbuka ghasia zilizotokea mjini Lagos wakati wakaazi wapatao milioni 15 wa jiji hilo walipoligeuza jiji hilo na kuwa uwanja wa mapigano:

| **1. Atmo** Lagos street scene (same sound for O-tone 6) |
|---|

| **2. Princess vehicles** |
|---|
| Kwanza nilipofika mjini Lagos, nilishangazwa sana na kila kitu nilichokiona mjini humo. Nilimuuza mamangu aliyenijibu kuwa hili ni jiji…Jiji la Lagos. Kwa kweli ni jiji kubwa. Mjini Lagos magari ni mengi na yanaendeshwa |

kwa kasi na katika hali ya hatari.Siku yangu ya kwanza kufika jijini niliogopa motokaa na malori.

**Narrator:**

Princess alihitaji muda zaidi kulifahamu nyema jiji na njia zake za mzingo, kinyume kabisa na kijijini Eldorado alikotoka! Jamaa zake ambao walikuwa maskini kiasi cha kushindwa kulisha familia yao walimruhusu kwenda kuomba omba barabarani. Muda si muda Princess alifahamu hatari ya kuzurura barabara za jijini, moja wapo ya miji hatari zaidi barani Afrika.

**3. Princess bus**

Kila siku kunapokuwa na msongamano wa magari, hukosi kusikia mlio wa risasi. Na kila mara wanapofyatua risasi, mimi hushikwa na uoga. Nilikuwa nikiwaona maafisa wa polisi wakikabiliana na majambazi waliojihami kwa kufyatuliana risasi barabarani. Niliogopa sana bunduki. Mara nyingine nikiwa kwenye basi na wanafyatuliana risasi, nilijaribu kuruka nje kupitia dirishani na hapo kujeruhiwa. Kama huwezi kutoroka kupitia lango la basi ni lazima uruke kupitia dirishani.

**Narrator:**

Kulala nje barabarani kwenye vipande vya maboksi pia kulikuwa na hatari zake, kwani tulivamiwa na majambazi wasio na aibu kuwapora watoto wadogo. Princess alishambuliwa mara kadhaa na mara nyingi kuporwa fedha zote alizokuwa nazo baada ya kuomba mchana kutwa.

**Princess gangs**

Wakati mwengine majambazi walikuwa wakinihangaisha na kuchukua pesa zangu zote kisha kutoroka. Lazima walikuwa wakiniona nikiomba mchana kutwa. Walichukua mfuko wangu wa plastiki uliokuwa na pesa na kutoroka. Nilikuwa nikipiga mayowe na watu walikuwa wakinisaidia baada ya kuwaarifu kwamba nimeibiwa. Walikuwa wakinisaidia na pesa kidogo kama nauli ya basi. Niliogopa, majambazi hao wa barabarani wangeliniua. Mara nyingine wakinitisha kunidunga kisu kabla ya kutoroka na pesa zangu. Nimeona watu wakidungwa visu na ndio sababu nikaogopa.

**Narrator:**

Watoto wanaorandanda mitaani mara nyigni hunyanyaswa, kuteswa, kupigwa, kubakwa au kutumiwa kama walanguzi. Princess alikuwa na bahati, hakukumbana na maovu yote haya, lakini alifahamu kwamba maisha yake yamo hatarini katika jiji hili la fujo. Ameshuhudia visa vingi vya ukatili.

**5. Princess people dying**

Nilipokuwa barabarani nilishuhudia visa vingi vya kikatili. Watu kunyang'anywa na kuuwawa na majambazi. Na ukithubutu kupiga mayowe wanakuchoma. Asubuhi nilikuwa nikiona maiti zimetapakaa barabarani. Niliona wake kwa waume wakiuawa. Mara nyingine majambazi hao pia waliuwawa kwa kuchomwa. Pia maiti za watoto wanaogongwa na magari wanapojaribu kuvuka barabara.

**Narrator:**

Baada ya kuanza kushuhudia visa vya ghasia jijini kila wakati, Princess alijutia maisha ya utulivu, usalama na raha kijijini mwake .

**6. Princess village**

Kwa kuwa mimi ni msichana mdogo, nilihisi maisha ya kijijini ni salama zaidi ikilinganishwa na ya jiji. Katika barabara za mji wa Lagos, hiyo ndio hali ya hatari ninayokumbana nayo kila siku. Watu waliniibia, kunibaka, kuniteka nyara, au hata kuniuza… ndizo hatari zilizomo katika barabara za jiji hili.

**Narrator:**

Licha ya yote hayo, Princess alimudu hali hiyo ngumu. Alifanikiwa kuwapata wasamaria wema waliokuwa tayari kumsaidia kutoka barabarani.

**7. Princess danger**

Wakati mwengine nilipokuwa barabarani watu nisiowafahamu waliniita na kuniambia niwafuate hadi nyumbani kwao, lakini nilikataa, kwa sababu nilishauriwa nisithubutu kufanya hivyo kwani baadhi yao ni wauaji wa kikatili. Na wengine hutaka kuwateka nyara wasichana wadogo na kuwafungia majumbani mwao kuwabaka. Nilipokuwa nikitembea baadhi ya niliokutana nao walinishauri niwe mwangalifu sana kwa sababu mimi ni msichana mdogo na wana hofu kwamba nimo hatarini.

**Narrator:**

Siku moja Princess akiwa katika shughuli zake za kuombaomba barabarani akiandamana na dadake mdogo walikamatwa na kupelekwa katika makao ya shirika linalopigana na biashara ya kuuza binadamu nchini Nigeria ***NAPTIP.***

| **8. Princess NAPTIP** |
|---|
| Tulikuwa katika shughuli zetu kuomba barabarani, maafisa wa serikali walikuja kutuhoji na kisha kutuweka ndani ya gari lao na kutupeleka moja kwa moja hadi ofisi za ***NAPTIP.*** |

**Narrator:**

Princess na dadake walizuiliwa katika ofisi hizo kwa zaidi ya miezi mitatu kabla ya kupata makao. Shukrani kwa shirika moja la kidini liitwalo ***TREM.***

| **9. Princess TREM** |
|---|
| Sasa naishi katika makao ya shirika hili la ***TREM*** mjini Lagos yanayomilikiwa na kanisa la Kiingili la Redeemed. Makao haya huwasaidia wanawake na wasichana wanaohitaji msaada wa dharura ambako hutunza kwa kupewa chakula, mavazi na matibabu. Maisha hapa ni mazuri ukilinganisha na yale ya barabarani. |

**Narrator:**

Tangu aingie katika mazingira haya mapya, maisha ya Princess yamenza kubadilika. Sasa amekuwa na mwelekeo na kupata marafiki wengi wapya.

Hii ni hatua ya kwanza katika kurejelea maisha yake ya kawaida. Lakini lazima akumbuke kwamba si rahisi kupata msaada wa aina hii au kutangamana na watu usiowajua hasa kwa mtu aliyeshuhudia maovu mengi kama alivyoshuhudia Princess. Hata hivyo hilo ndilo jukumu la makao hayo – kuwaelimisha watu na kuwapa muongozo wa kuweza kuishi tena maisha bora katika jamii.

**10. Atmo pots+ Princess**

Katika makao haya, huwa tunagawana majukumu. Siku ya Jumapili huwa ni siku yangu kuosha vyombo na usafi wa nje.

**11. Atmo church**

**Narrator:**

Pia siku hiyo ya Jumapili ni siku ya Princess kwenda kanisani. Huwa siku muhimu sana kwake.

**12. Princess Sunday**

Siku ya Jumapili huchukuliwa na kupelekwa hadi makao makuu ya kanisa hilo la Redeemed ili kuhudhuria ibada ya vijana.

**13. Atmo school**

**Narrator:**

Mara nyingi si rahisi kwa mtoto aliyekuwa chokora pipa kurejelea maisha ya kawaida kutangamana tena na jamii. Baadhi yao huendelea kuandamwa na kiwewe cha maisha ya uchokora pipa hata wakiwa watu wazima. Lakini sheria kuhusu haki za watoto zinahimiza haki ya kila mtoto kupata elimu, na kuishi kama watoto wengine miongoni mwa jamii. Hata hivyo mataifa mengi ulimwenguni bado yanakumbwa na hali ngumu ya kiuchumi na kijamii na hivyo kushindwa kulipa kipaumbele suala la watoto wanaorandaranda mitaani.

**13. Atmo school**

**Narrator:**

Shirika la ***TREM*** hutoa msaada wa masomo na hivyo kumpa Princess matumaini makubwa maishani baada ya kujiunga na shule moja iliyoko kitongoji cha mji wa Ketu. Sasa anamatumaini ya kutimiza ndoto yake siku za usoni.

**14. Princess actress**

Nataka kuwa muigizaji kwasababu baadhi ya filamu ninazotazama huwaona watu wakuongea lugha ya kiingereza katika hali inayonitamanisha sana. Hupenda wanavyoigiza ,wanavyotembea, ndio sababu nataka kuwa kama wao. Ninafurahi kwamba sasa nimetoka katika

maisha ya kuombaomba barabarani. Niko nyumbani sasa na ni fursa nzuri ya kuniwezesha kutimiza ndoto yangu maishani. Singeweza kutimiza ndoto hiyo kama ningekuwa bado niko barabarani. Nikiwa muigizaji itakuwa rahisi kwangu kuwasaidia wazazi wangu kuliko maisha ya kuomba omba barabarani.

**End music**

**OUTRO :**

Hiyo ilikuwa ripoti iliyoandikwa na Sam Olukoya kutoka nchini Nigeria Tumefika mwisho wa kipindi cha leo Noa Bongo Jenga maisha yako. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao manwani yetu ni www.dw-world.de/lbe Ungana nasi tena kwa makala mengine wakati mwengine. Kwaheri kwa sasa!

**Music**